# IBADA

## BINAFSI YA SIFA



James Kalekwa

# IBADA BINAFSI YA SIFA.

James Kalekwa

# Orodha ya Yaliyomo

**Tabaruku**....................................................................4

**Salamu na Utangulizi**....................................................5

Sura ya Kwanza:..............................................................7

*Uelewa muhimu kuhusu Ibada ya Sifa*................................7

SURA YA PILI:..................................................................16

*Muda Mzuri wa Ibada ya Sifa*...........................................16

Sura ya Tatu:....................................................................19

*Mtiririko wa Sifa*............................................................19

9. Jehovah Sabaoth - "Bwana wa Majeshi"............... 30

10. Jehovah Shalom - "Bwana wa Amani yetu"...... 31

11. Jehovah Shammah - "Bwana yupo hapa".......... 31

Abba - "Papa" or "Baba"...............................................32

Adonai - "Bwana" or "Mwalimu"..................................32

Alpha & Omega - "Mwanzo na Mwisho"......................33

Immanuel - "Mungu pamoja nasi"................................33

Yeshua (Yesu) - "Mungu wokovu wangu"....................33

SURA YA NNE:............................................................ 37

*Nani Amsifu Mungu?*................................................. 37

# Tabaruku

Mfululizo wa vitabu hivi vya kieltroniki (e-books) bure kwa kila atakaye; ni himizo la kiungu ndani yangu kuujaza ulimwengu kwa maarifa ya utukufu wa Mungu kama maji yaifunikavyo bahari.

Ninatabaruku kitabu hiki kwa kanisa la Kristo na kwa nchi yangu niipendayo, Tanzania.

Kanisa litashinda na kushamiri zaidi!

Tanzania, ninakupenda kwa moyo wote!

# Salamu na Utangulizi

Mfululizo huu wa vitabu vya kieletroniki ni maono ambayo Mungu ameweka ndani ya mtumishi wake, mume wangu mpenzi, kama namna yake ya kuonyesha shukurani kwa Mungu kwa zawadi ya maisha.

Ninamfahamu mume wangu kama mtu anayempenda Mungu kupitiliza. Yuko tayari kulipia gharama yoyote ile kuonyesha hilo. Ni mtu anayewapenda watu wa Mungu kwa namna ambayo sijawahi kuona. Yamekuwa ni maombi yake kuyagusa maisha ya wengi kwa kadiri inavyowezekana kabla Yesu Kristo hajarudi.

Anapoadhimisha siku ya kuzaliwa kwake, amekuandikia kitabu hiki, akapangilia na kufanya kipatikane kwako bila malipo yoyote. Nimemwona anvyokesha; wakati mwingine kuamka alfajiri sana au kuchelewa sana kulala ili kukamilisha uandishi. Nimemuona anavyoomba na kuombea wasomaji, anavyojisomea na kutafiti ili kuhakikisha anafanya uwasilishaji wa thamani.

Ningependa tuthamini zawadi hii ambayo sisi wengine tunanufaika nayo bila kulipia gharama:

1. Mshukuru Mungu pamoja nasi kwa zawadi hii ya maisha ya Pastor James Kalekwa kisha muombee maisha marefu na afya njema.
2. Mwandikie ujumbe wa kumsalimu na kumpongeza ukisema ni kwa namna gani

huduma yake imeyagusa maisha yako. Ninajua hili litaufurahisha sana moyo wake.

3. Wafikishie vitabu hivi walau watu hamsini tu. Ni vitabu vinatolewa bila malipo (vimeyagharimu maisha ya mwandishi ili vikufikie).
4. Usiuze vitabu hivi. Tuligundua kuwa kuna watu wanavisambaza kwa malipo ya fedha. Hiyo si sawa. Itakuwa ni kwa hasara yako mwenyewe ukifanya hivyo.

Baada ya kuyasema hayo, nikuhakikishie ya kwamba mtu huyu mkuu wa Mungu amejaa hekima za kiungu na neno ambalo siku zote hutokeza shuhuda maishani mwa wengi. Kwa kusoma kitabu hiki, ushuhuda wako unafuatia. Nikutakie usomaji mwema.

Na heri ya kuzaliwa kwa mpendwa wetu, zawadi ya mbingu kwenye kizazi chetu, Pastor JK.

Frida James Kalekwa (Mama Pastor JK)
Mke wa mwandishi
Juni, 2023
Dodoma, Tanzania

# Sura ya Kwanza:

*Uelewa muhimu kuhusu Ibada ya Sifa*

Yona alikaa kwenye tumbo la samaki siku 3 mfululizo - usiku na mchana (Yona 1:17).

> "BWANA akaweka tayari samaki mkubwa ili ammeze Yona, ***naye Yona akawa ndani ya tumbo la samaki yule muda wa siku tatu, mchana na usiku.***"

Biblia haisemi moja kwa moja swala la kula na kunywa… na huduma zingine muhimu kwa mwili wa mwanadamu (maswala ya kujisaidia, kupumzika/kulala) - lakini ndani ya tumbo la samaki hakuna kula wala kunywa ISIPOKUWA kama kuna muujiza ambao BWANA alifanya - hata hivyo Biblia haisemi pia.

Siku tatu kwenye mazingira "katili" sana kwa maisha ya mwanadamu.

Bwana Yesu anarejelea tukio hili ili kutengeneza uelewa kwa watu wanaomsikia kwa kuwa wanafahamu tukio la Yona. Analinganisha mazingira ya Yona na ya kwake.

> *“**Kwani kama vile Yona alivyokuwa** siku tatu mchana na usiku katika tumbo la nyangumi, **hivyo ndivyo Mwana wa Adamu atakavyokuwa** siku tatu mchana na usiku katika moyo wa nchi.”*
> Mathayo 12:40

Wakati ninasoma andiko hili kwa mara ya kwanza nilikuwa ninawahi sana kuona swala la muda, yaani, idadi ya siku tatu. Lakini baada ya kuendelea kujifunza kwa kuomba hapo nikapokea ufahamu ya kwamba hata mazingira. Ukatili wa mazingira aliyoyapitia Yona ni kama vile alikuwa amekufa. Hajui chochote kinachoendelea kwenye dunia ya walio hai; hajui kuhusu muda; hana mawasiliano na ndugu zake; hawezi kujongea kwenda popote… siyo tu kwamba alipoteza maisha yake ya kawaida bali alipoteza maisha yake! Alikuwa amekufa.

Hata hivyo, Yona aligundua mapema ya kwamba kuna jambo haliko sawa. Kimsingi anapaswa kufahamu kwa sababu tangu mwanzo wa safari alijua anatakiwa kufanya nini, lakini yeye akaamua kutenda tofauti. Hana

wa kumlaumu. Anakubaliana na mtokeo ya kutokutii kwake.

> *"Basi neno la BWANA lilimjia Yona, mwana wa Amitai, kusema,* ***Ondoka, uende Ninawi****, mji ule mkubwa, ukapige kelele juu yake; kwa maana uovu wao umepanda juu mbele zangu.* ***Lakini Yona akaondoka akimbilie Tarshishi, apate kujiepusha na uso wa BWANA;*** *akatelemka hata Yafa, akaona merikebu inayokwenda Tarshishi; basi,* ***akatoa nauli****, akapanda merikebuni, aende pamoja nao Tarshishi,* ***ajiepushe na uso wa BWANA.****"* Yona 1:1-3

Kutokea kwenye maandiko hayo utaona maelekezo kutoka kwa Bwana yalivyokuwa wazi sana. Lakini Yona akatenda kinyume na maelezo. Kuna neno linajirudia kwenye mistari hiyo kama sababu kuu ya kutenda kinyume na maelekezo ya Mungu, "… apate kujiepusha na uso wa BWANA."

Moja kati ya malengo ambayo mtu hawezi kuyafikia na kuyatimiliza kwa ukamilifu ni lengo la kumkimbia Bwana. Haliwezi kufanikiwa! Wakati ninasoma kitabu

hiki, nilikuwa ninamsikia mzaburi akicheka kwa dhihaka moyoni mwangu kuhusu lengo hili batili.

> *“Niende wapi nijiepushe na roho yako?*
>
> *Niende wapi niukimbie uso wako?”* Zaburi 139:7

Baada ya ugunduzi huo, mwitikio wake ukawa ni maombi - kama ambavyo kwa haraka wengi wetu tungeitikia.

> *“Ndipo Yona akamwomba BWANA, Mungu wake, katika tumbo la yule samaki,”* Yona 1:1

Hata hivyo unafanya nini sasa kwenye tumbo la Samaki zaidi ya kuomba? Ninataka kukuhakikishai mtu wa Mungu ya kwamba huwa kuna mazingira mabyo kuona siyo chaguo mojawapo tena bali linabaki kuwa chaguo pekee. Kuna kibano ambcho Mungu anaruhusu ukipitie ili ukome “kujiepusha na uso wa Bwana!”

Yona akaomba ndani ya tumbo la samaki (Yona 2:1-8); Aliomba kwa muda gani? kwa siku 3 mfululizo, usiku na mchana... Mawazoni mwangu ninamuona anaomba halafu anapumzika, anaomba halafu anapitiwa usingizi... anaomba halafu anakaa au analala... vyovyote vile lakini

ninachojua yale mazingira aliyokuwamo hakuwa na "issue" ya kufanya isipokuwa KUOMBA!

Baada ya maombi yote hayo yote, hakukuwa na matokeo. Ni kama mbingu zilikuwa kimya dhidi yake. Unafanya nini pale ambapo mbingu zinaonekana kuwa kimya?

ISIPOKUWA alipobadili gia. Akaamua kufanya jambo tofauti kidogo na kuomba tena aina ya maombi aliyokuwa akiyafanya (soma mstari 2-8).

> "Lakini mimi ***nitakutolea sadaka kwa sauti ya shukurani***; Nitaziondoa nadhiri zangu. ***Wokovu hutoka kwa BWANA.***" Yona 2:9

Aliachilia sadaka yake ya midomo kwa sababu anasema "sadaka kwa sauti..." Hii siyo sadaka ya vitu au fedha. Aliachilia shukurani kwa midomo yake. Neno la Mungu linatufundisha kuhusiana na aina hii ya utoaji wa sadaka.

> "Basi, kwa njia yake yeye, ***na tumpe Mungu dhabihu ya sifa daima, yaani, tunda la midomo iliungamayo jina lake.***" Waebrania 13:15

Dhabihu ya sifa inafafanuliwa na mwandishi wa kitabu cha Waebrania kuwa ni tunda la midomo iliungamayo

jina lake. Kuungama ni kukiri… kusema waziwazi bila hali ya kificho.

Baada ya kusema shukurani zake anahitimisha kwa sifa WOKOVU HUTOKA KWA BWANA... WOKOVU NI WA BWANA! Anaungama… anasema na kukiri waziwazi. Ukilinganisha na aina ya maombi ambayo amekuwa akiyaomba kwenye kistari iliyotangulia; utaona amehama kutoka kwenye laumu na masimulizi kwenda kwenye shukurani na sifa.

Mara tu baada ya kubadilisha namna ya kumuelekea Mungu kwenye hali ya mazingira yale katili… mara moja tunaona mazingira yanamuitikia kwa Mungu kuingilia kati.

> "BWANA akasema na yule samaki, naye akamtapika Yona pwani." Yona 2:10

Sasa, ukiwa kwenye hiyo hali uliyomo BADILI GIA... Anza kumsifu Mungu. Kwenye mazingira katili... msifu Mungu... kwenye mazingira yasiyo rafiki msifu Mungu... baada ya siku tatu za kuomba na kuona majibu ya maombi yako "yamechelewa" msifu Mungu!

Achilia dhabihu yako ya sifa, yaani, tunda la midomo inayoliungama jina la BWANA.

Wokovu ni wa BWANA!

Wokovu ni wa BWANA!

WOKOVU NI WA BWANA!

Na hilo ndilo neno la Mungu!

Huwa ninawaambia watu ufunguo wat umbo la samaki mkubwa namna ile ni sifa. Si lazima kila samaki umpasue tumbo. Si lazima uzungumzie hali ya giza na ukatili wa mazingira ya tumbo la samaki… si lazima! Jielekeze kwa Mung utu… elekeze tunda la midomo yako kwa BWANA. Kwa sababu ni kweli kabisa "Wokovu ni wa BWANA!"

Ukikutana na Mungu anatafuta (nimeongea kibinadamu), basi anatafuta aina ya watu kwa aajili ya tukio hili maalum.

Anatafuta WAABUDU HALISI (Maana yake waabudu ni wengi) ili WAMWABUDU!

> *“Lakini saa inakuja, nayo sasa ipo, ambayo waabuduo halisi watamwabudu Baba katika roho **na kweli**. Kwa maana Baba awatafuta **watu kama hao** wamwabudu.”* Yohana 4:23

Mpendwa wangu, unatafutwa. Watu kama hao ni adimu ndiyo maana hata Mungu anawatafuta. Kwa usomaji wa kitabu hiki nimeona katika roho ya kwamba hekima imeingia na kuzama ndani yako kiasi cha kukusababisha upatikane kwenye ibada ya sifa.

Ooooh! Kabla sijahitimisha sura hii. Roho Mtakatifu amenikumbusha jambo… Yona alikuwa mweyewe, yaani, peke yake kwenye tumbo la samaki. Hakuwa kwenye tamasha, kusanyiko la ibada; hakuwa na wapigaji wa vyombo wala kwaya; hakuna na mwongozaji wala waitikiaji; hakuwa na kiongozi wa uchezaji “choreography” wala muongozaji wa uimbaji… Ni ibada binafsi.

Hebu fikiria sasa kwenye ibada moja wamekuja “Mayona” kama arobaini hivi? Wenye uelewa huu wa shukurani na sifa!

Ibada hii inaanza na wewe binafsi. Inaanzia moyoni mwako. Inaanza kwa kuifahamu kweli. Kisha unaitenda na kuitekeleza mwenyewe. Mkikutana kwenye kusanyiko la waamini, inakuwa ni kama kuchochea tu kuni za moto wa shukurani na sifa siyo kuanza.

Kule kwneye tumbo la samaki huna wa kumuonyeshea shukurani na sifa zako isipokuwa BWANA tu… si unajua hivyo? Huo ndiyo uwe ukweli unaokuendesha linapokuja swala la ibada ya sifa. Sina mtazamaji au msikilizaji yeyote wa sifa nitoazo zaidi ya BWANA.

## SURA YA PILI:

*Muda Mzuri wa Ibada ya Sifa*

Kwa kuwa umeelewa sana sura ya kwanza ya kitabu hiki. Ni kama vile umetamani kuacha kusoma ili ufanye utekelezaji wa neno. Na wengine ndivyo walivyotenda wakati wanaendelea kukisoma. Kuna swali muhimu hapa la kujiuliza NINAPASWA KUMSIFU MUNGU MUDA GANI?

> *"Nitamhimidi Bwana **kila wakati**, Sifa zake zi kinywani mwangu DAIMA."* Zaburi 34:1

> *"Basi, kwa njia yake yeye, na tumpe Mungu dhabihu ya sifa **DAIMA**, yaani, tunda la midomo iliungamayo jina lake."* Waebrania 13:15

Kwenye makusanyiko ya ibada tunaweza kuwa na "kipindi/wasaa" wa SIFA... ili kumpa nafasi mwamini kuungana na waamini wenzake kutoa sadaka zao za midomo iliungamayo jina lake – SIFA!

Tunaweza kuwa na ibada iliyotengwa maalum kwa ajili ya kutoa sadaka ya sifa tu! Watu wa Mungu wakaja pamoja na kuongozwa na mtu mmoja au kundi la waimbaji… ni sawa! Neno la Mungu limetutaka kuwa kwenye mtiririko wa kiutaratibu kila tukusanyikapo.

Kipindi kitaisha, wasaa utakoma, ibada maalum, tamasha, mkesha utaisha... Je, sifa zinapaswa kuisha?

Nimeitwa kumsifu Mungu DAIMA.

DAIMA ni siku zote

DAIMA ni kila siku

DAIMA ni muda wote

Ni kila saa, kila wakati, ni kwa uendelevu, ni tena na tena.

SIFA ni sadaka inayotolewa kwa midomo. Kwa kuwa hakuna muda ambapo huwa unauvua mdomo wako au unatenganishwa na mdomo wako, basi hii ni sadaka ya muda wote.

Kipindi cha sifa kikiisha – endelea kusifu!

Tamasha la sifa likiisha – endelea kusifu!

Wasaa wa sifa ukiisha – endelea kusifu!

Mwezi wa sifa ukiisha – endelea kusifu!

Ni DAIMA!

Angalia mpendwa wangu, mtu anayemsifu Mungu kila wakati; daima. Ni mtu ambaye hatahangaika kumsifu Mungu kwenye kusanyiko la waaminio. Huwa ninaambia watu, ukiona kuna mwamini anahangaika kumfanyia Bwana sifa awapo kwenye kusanyiko, hicho ni kiashiria cha uduni wa maisha binafsi ya sifa.

Na hilo ndilo neno la Mungu.

## **Sura ya Tatu:**

*Mtiririko wa Sifa*


Kwa kuwa umeelewa vyema sura ya pili ya kitabu hiki. Ninakuona katika roho unamsifu Bwana kila eneo na kila wakati. Siku moja tutakutana uwanja wa ndege na tutasalimia kwa sifa vinywani mwetu; siku moja tutaonana ibadani na tutasemeshana kwa sifa; ipo siku tutakutanishwa ofisini na tutatazaman huku tumejawa sifa; ninaona katika roho kuna watakatifu tutakutana kwenye vikao na mabaraza na kudhani tumesalimiana kumbe tulikuwa tunatoa dhabihu za sifa… na bado tutaelewana!

Lengo langu kwenye sura hii ni kukuonyesha mtiririko mmojawapo uliomo kwenye maandiko matakatifu kuhusiana na maswala ya kumwendea Bwana hususani katika eneo la sifa.

Tunatambulishwa na mmoja wa watu waliokuwa "vichaa" linapokuja swala la kumsifu Mungu. Huyu alikuwa ameuzwa jumla.

> "Ingieni malangoni mwake **kwa kushukuru;** Nyuani mwake **kwa kusifu**; Mshukuruni, **lihimidini jina lake**;"
>
> Zaburi 100:4

Mwandishi wa Zaburi anaandika mtiririko huu akijikita kiuelewa kutokea kwenye muundo hekalu:




(Picha imepakuliwa kutoka mtandaoni: https://theinvisiblelivingword.wordpress.com/2014/09/15/the-jerusalem-temple-was-left-desolate-the-shadow-was-replaced-with-the-reality/)

Kwenye hekalu kulikuwa na malango ambayo mtu akiyapita ndiyo huingia kwenye nyua (courts).

I. Malangoni kwa KUSHUKURU – Mzaburi anatengeneza taswira mawazoni mwetu kama vile unatembea kutokea nyumbani kuja hekaluni. Ili uweze

kupita kwenye malango uingie ndani, unafanya shukurani. Ni hali ya kutambua ya kwamba aliyekuleta umbali huo ni BWANA mwenyewe; kufika kwenye malango ya hekalu nayo ni neema. Kwa hiyo, mwitikio wako unapaswa kuwa wa shukurani. Kushuruni nini basi? Ni kuutambua (acknowledge) wema wa Bwana kwenye maeneo yote ya maisha yako. Unafanya tathmini na tafakari kuhusu maisha yako na maisha tu kwa ujumla halafu unaona ni kwa jinsi gani Mungu amekufadhili na kukusaidia pakubwa namna ile. Kwanza, unamshukuru Mungu kwa vile alivyo kwa ujumla na vile alivyo kibinafsi kwenye maisha yako na mambo yanayohusiana na wewe.

Utagundua ya kwamba kwa kadiri unavyozidi kushukuru. Unaongeza kushukuru. Utagundua ya kwamba mambo ya kumshukuru Mungu ni mengi sana. Orodha yako ya shukurani inaweza kuchukua miezi mitatu bila mapumziko kuimaliza.

> "Ee BWANA, Mungu wangu, umefanya kwa wingi; Miujiza yako na mawazo yako kwetu;

Hakuna awezaye kufananishwa nawe;
Kama ningependa kuyatangaza na kuyahubiri,
**Ni mengi sana hayahesabiki.**"
Zaburi 40:5

Ni kweli kushukuru ni kutaja mambo kimahususi na kutambua wema wa Bwana kwenye hayo. Lakini kwa kadiri unavyoendelea, badala ya kutaja nyakati, watu, matukio, ameneo ambayo unamshukuru Mungu kwa sababu ni mengi n.k ambayo Bwana alikuponya; moyo wako uliofurika shukurani unajikuta unayajumlisha mambo yote yanayohusiana na UPONYAJI na kuyataja kwa pamoja - BWANA WEWE NI MPONYAJI WANGU, AFYA MIFUPANI MWANGU, UZIMA WA MWILI WANGU...

Hausemi tena jambo moja moja bali unayakusanya na kuyafunga kwenye kundi moja la maelezo ambalo kimsingi linamwelezea BWANA kuwa ni nani kwako kuhusiana na ajenda hizo.

Na hapo ndipo unagundua umeibukia kwenye SIFA!!!

II. Nyuani mwake kwa KUSIFU – Kwa kurejelea ule muundo wa hekalu. Utaelewa sasa umeingia kwenye ukumbi au lugha ya Biblia inayotumika ni nyua! Ukiingia nyuani kinywa chako kinakuwa kimejaa maelezo kumuhusu BWANA tu… Kumbuka hii ni safari kuelekea patakatifu pa patakatifu kule kwenye hekalu. Sifa ni kuutambua UKUU WA BWANA.

Sawa... iko hivi, sifa ni matokeo ya moyo uliojawa na shukurani. Kama huwezi kumshukuru Mungu, huwezi kumsifu!

Kwa hiyo, SIFA inatiririkia kutokea kwenye moyo wa SHUKURANI.

Kusifu ni kuutambua UKUU WA MUNGU: kwa majina yake, kwa matendo yake (uweza wake) na kwa vile alivyo.

Kuna namna nyingi za kumsifu Mungu, hapa kwenye kitabu hiki nitashirikisha namna tatu tu:

**a) Kwa vile alivyo**

Unakumbuka kwenye tenzi iitwayo "Bwana Mungu Nashangaa", mwandishi anatoa sababu ya kusifu kwake kwenye kiitikio:

> *Roho yangu na ikuimbie*
>
> *Jinsi wewe ulivyo mkuu*

Kwenye beti za wimbo anaelezea matendo, kazi za mikono na mambo mengine mengi. Lakini hitimisho lake ni kwamba sababu ya sifa ni vile Mungu alivyo – Mkuu!

Yehovah ni Mungu ambaye hahitaji afanye chochote ndiyo umsifu. Vile alivyo anastahili tu kusifiwa. Ni mkuu… ni wa ajabu… wa kushangaza!

Mtunzi mmoja aitwaye Chris Tomlin kila akijaribu kuelezea kisayansi kazi ya uumbaji na mchakato ambao Mungu alifanya wakati anaumba, anaishia kusema Usiyeelezeka! Indescribable.

> Indescribable, uncontainable,
> You placed the stars in the sky and You know them by name.
> You are amazing God

All powerful, untameable,
Awestruck we fall to our knees as we humbly proclaim
You are amazing God

Hiyo ndiyo namna ya kumsifu Mungu huyu asiyelezeka.

### b) Kwa majina yake

Njia mojawapo ya kumsifu Mungu kwa kutaja na kutangaza majina yake. Mungu ni mmoja lakini jinsi anavyojifunua kwa mtu fulani au kundi la watu kwa namna halisi sana kiasi kwamba watu hao humtaja Mungu kwa jina fulani. Hilo jina linaonyesha uelewa wa watu kuhusu eneo ambalo Mungu amejifunua kwao. Kwa hiyo, kutaja jina la Mungu ni kutaja sifa za Mungu.

Kwenye maandiko matakatifu, utagundua ya kwamba, wanafunzi waliishi na kumfahamu Bwana Yesu kwa kiwango au daraja fulani. Ni mpaka pale alipofunua upande wake fulani ndipo wakabaki wanashangaa tu ili hali wamekuwa naye muda wote huo wa maisha yao.

Baadhi ya majina ya Mungu na maelezo kuhusiana na sifa zake:

### 1. Elohim

**Mwanzo 1:1** – "Hapo mwanzo Mungu (Elohim) aliziumba mbingu na nchi."

Maelezo: Mwenye uweza (kuna tofauti kati ya uwezo na uweza), Wingi wa "El" ikielezea Utatu Mtakatifu - 3 in 1

Maandiko mengine ya rejea kuhusu Elohim:

- Mwanzo 17:7
- Kutoka 20:23
- Isaya 41:10
- Yeremia 31:33

**2. El shaddai**

Genesis 17:1 – *"Abramu alipokuwa mtu wa miaka tisini na kenda, BWANA akamtokea Abramu, akamwambia, Mimi ni Mungu Mwenyezi (El Shaddai), uende mbele yangu, ukawe mkamilifu."*

Maelezo: Mwenye uweza wote, Utoshelevu, Mmiliki wa vyote.

Maandiko mengine ya rejea kuhusu El Shaddai:

- Mwanzo 49:24
- Zaburi 132:2,5
- 2 Wakorintho 12:9

### 3. El Elyon

Mwanzo 14:20 *"Ahimidiwe Mungu Aliye juu sana (El Elyon), aliyewatia adui zako mikononi mwako. Abramu akampa fungu la kumi la vitu vyote."*

Maelezo: Yuko juu ya yote, Mwenye hatimiliki ya Ubwana, Mamlaka

Maandiko mengine ya rejea kuhusu El Elyon:

- Hesabu 24:16
- Kumbukumbu la Torati 26:19
- 2 Samwel 22:14
- Zaburi 9:2
- Danieli 3:26

### 4. El Roi

Mwanzo 16:13 "Akaliita jina la BWANA aliyesema naye, Wewe U Mungu uonaye, kwani alisema, Hata hapa nimemwona yeye anionaye (El-Roi)?"

Maelezo: Anayejua yote, Umakinifu

Maandiko mengine ya rejea kuhusu El Roi:

- Kutoka 2:25
- Zaburi 139:11
- Mathayo 6:4
- 1 Petro 3:12

5. *Majina mengine ya Mungu kama "El" kwenye Biblia:*

- El Chaiyai - "Mungu ni Uhai wangu - Zaburi 42:8
- El Chanuun - "Mungu wa huruma" - Yona 4:2, Nehemia 9:31
- El Gibhor - "Mungu mwenye nguvu aokoaye", "Shujaa" - Isaiaya 9:6, Yeremia 32:17-18
- El Olam - "Mungu adumuye", "Mungu wa milele" - Mwanzo 21:33, Zaburi 90:1-3
- El Oseh Phela - "Mungu atendaye maajabu" - Zaburi 77:14
- El Qanna - "Mungu mwenye wivu" - Kutoka 20:5
- El Simchath Giyl - "Mungu wa furaha yangu kuu" - Zaburi 43:4
- El Hakkadosh - "Mungu mtakatifu" - Isaya 40:25
- Ha El Hanne' Eman' - "Mungu mwaminifu" – Kumbukumbu la Torati 7:9
- Elohei Chasdi - "Mungu wa upendo na ukarimu mkuu" - Zaburi 59:10,17
- Elohei Mikkarov - "Mungu aliye karibu" Yeremia 23:23
- Elohim Chayim - "Mungu aliye hai" - Yoshua 3:10
- Elohim Yachal - "Mungu wa tumaini" - Warumi 15:13
- Elohim Emet - "Mungu wa kweli" - Yeremia 10:10

## 6. Yehova Yire

Mwanzo 22:14 *"Ibrahimu akapaita mahali hapo **Yehova-yire**, kama watu wasemavyo hata leo, Katika mlima wa BWANA itapatikana."*

7. **Yehova Nissi**

Kutoka 17:15 "Musa akajenga madhabahu, akaiita jina lake Yehova-nisi (Bendeara ya ushindi wangu);"

8. **Yehova Rafa**

Kutoka 15:26 "akawaambia, Kwamba utaisikiza kwa bidii sauti ya BWANA, Mungu wako, na kuyafanya yaliyoelekea mbele zake, na kutega masikio usikie maagizo yake, na kuzishika amri zake, mimi sitatia juu yako maradhi yo yote niliyowatia Wamisri; kwa kuwa **Mimi ndimi BWANA nikuponyaye**."

9. **Jehovah Sabaoth** - "Bwana wa Majeshi"

Isaya 1:24 "Kwa hiyo, asema Bwana, BWANA wa majeshi, Mwenye enzi, wa Israeli, Nitapata faraja kwa hao

wanipingao, nitatwaa kisasi kwa adui zangu;″

10. **Jehovah Shalom** - "Bwana wa Amani yetu"

Waamuzi6:23-24 "BWANA akamwambia Amani iwe pamoja nawe; usiogope; hutakufa. Ndipo Gideoni akamjengea BWANA madhabahu hapo, akaiita jina lake, Yehova-Shalomu"

11. **Jehovah Shammah** - "Bwana yupo hapa"

Ezekiel 48:35 "Kuuzunguka ni mianzi kumi na nane elfu; na jina la mji huo tangu siku hiyo litakuwa hili, BWANA yupo hapa."

12. Majina mengine ni pamoja na:

- Jehovah Baal Perez - "Bwana wa mpenyo" - 2 Samweli 5:20
- Jehovah Kesel - "Bwana ujasiri wangu" - Mithali 3:26
- Jehovah Mephalti - "Bwana mwokozi wangu." - Zaburi 32:7
- Jehovah M'Kaddesh - "Bwana atakasaye" - Ezekieli 37:28

- Jehovah Rohi or Raah - "Bwana mchungaji wangu" -Zaburi 23:1
- Jehovah Shomreka - "Bwana mtunzaji wangu" - Zaburi 71:5
- Jehovah Tsaba - "Bwana shujaa wetu" - 1 Samweli 17:45
- Jehovah Tsidkenu - "Bwana haki yetu" - Yeremia 23:6
- Jehovah Tsuri - "Bwana mwamba wangu" - Isaya 26:4

Abba - "Papa" or "Baba"

> Marko 14:36 "Akasema, Aba, Baba, yote yawezekana kwako; uniondolee kikombe hiki; walakini, si kama nitakavyo mimi, bali utakavyo wewe."

> Warumi 8:15 "Kwa kuwa hamkupokea tena roho wa utumwa iletayo hofu; bali mlipokea roho ya kufanywa wana, ambayo kwa hiyo twalia, Aba, yaani, Baba."

Wagalatia 4:6 Na kwa kuwa ninyi mmekuwa wana, Mungu alimtuma Roho wa Mwanawe mioyoni mwetu, aliaye, Aba, yaani, Baba.

**Adonai** - "Bwana" or "Mwalimu"

Mwanzo 15:1 "Baada ya mambo hayo neno la BWANA likamjia Abramu katika njozi, likinena, Usiogope,

Abramu, Mimi ni ngao yako, na thawabu yako kubwa sana."

Hesabu 14:17 Basi sasa nakusihi sana, uweza wa Bwana wangu na uwe mkuu, kama ulivyonena, uliposema,

**Alpha & Omega** - "Mwanzo na Mwisho"

Isaiah 44:6 "BWANA, Mfalme wa Israeli, Mkombozi wako, BWANA wa majeshi, asema hivi; Mimi ni wa kwanza, na mimi ni wa mwisho; zaidi yangu mimi hapana Mungu."

Ufunuo 21:6- ″Akaniambia, Imekwisha kuwa. Mimi ni Alfa na Omega, Mwanzo na Mwisho. Mimi nitampa yeye mwenye kiu, ya chemchemi ya maji ya uzima, bure.

**Immanuel** - "Mungu pamoja nasi"

Isaya 7:14 ″Kwa hiyo Bwana mwenyewe atawapa ishara. Tazama, bikira atachukua mimba, atazaa mtoto mwanamume, naye atamwita jina lake Imanueli."

Mathayo 1:23 "Tazama, bikira atachukua mimba, Naye atazaa mwana; Nao watamwita jina lake **Imanueli**; Yaani, Mungu pamoja nasi."

**Yeshua** (Yesu) - "Mungu wokovu wangu"

Mathayo 1:21 "Naye atazaa mwana, nawe utamwita jina lake Yesu, maana, yeye ndiye atakayewaokoa watu wake na dhambi zao."

### c) Kwa matendo yake

Linapokuja swala la matendo ya Bwana, kwanza, ni matendo yake kwa ujumla kwa uumbaji wake kisha kwako binafsi. Sasa, matendo ya Bwana kwako binafsi ni wewe ndiye ambaye unayajua kwa kina. Wewe na Bwana mnajuana mlikotoka.

Nigusie kidogo tu kuhusu matendo ya Bwana kwa ujumla:

> *"Je! Mungu hupotosha hukumu?*
>
> *Au, huyo Mwenyezi hupotosha yaliyo ya haki?"*
>
> Zaburi 8:3
>
> *"Mbingu zauhubiri utukufu wa Mungu,*
>
> *Na anga laitangaza kazi ya mikono yake."* Zaburi 19:1

Kwenye kitabu cha Zaburi utaona sana mtindo huu wa kumsifu Mungu kwa utendaji wake wa ujumla. Ngoja nikuonyeshe moja ya nyimbo ninazozipenda sana kwenye neno la Mungu… huu ni wimbo ambao taifa zima liliimba… watu zaidi ya laki sita (600,000) wanaimba kwa wakati mmoja bila kuwa na mazoezi au

maandalizi ya uimbaji huo. Matendo ya Bwana yameonekana, nao wakalipuka kwa moyo wa sifa!

> *"Ndipo Musa na wana wa Israeli wakamwimbia BWANA wimbo huu wakanena, na kusema,*
>
> *Nitamwimbia BWANA, kwa maana ametukuka sana; Farasi na mpanda farasi amewatupa baharini."* **Kutoka 15:1**
>
> *"Miriamu akawaitikia, Mwimbieni BWANA kwa maana ametukuka sana; Farasi na mpanda farasi amewatupa baharini."* **Kutoka 15:21**

Moja ya vitabu kwenye maandiko matakatifu vitakavyokusaidia kuyajua matendo ya Mungu kwa ujumla ni kitabu cha Zaburi. Hata hivyo, wimb kama hyuo wa wana wa Israeli kwenye kitabu cha Kutoka unaweza kukutengenezea mfano wa muundo wa kumsifu Bwana kwa kuelezea na kuyatangaza matendo yake!

Sasa, sifa inapoufurisha moyo wako... utagundua pia kila ukimtafakari Mungu na ukitafuta neno zuri la lugha yako au maelezo mazuri kuelezea kile kilichoujaza moyo wako, unagundua havitoshei.

Unajikuta ukitumia mikono yako, magoti yako, machozi yako, kelele zako, kilio chako... unalala chini, unaanguka

kifudifudi, unanyanyua mikono juu, unamwaga machozi... huna maneno toshelevu.

Na hapo ndipo safari ya KUABUDU huanzia!

Na hilo ndilo neno la Mungu!

Mungu akupe neema ya kumshukuru mpaka moyo wako ufurike kiasi cha kuingia kwenye sifa..  na upokee neema ya kusifu kiasi cha kukosa lugha na maneno toshelevu ili uingie kuabudu... katika Jina la Yesu Kristo!

# SURA YA NNE:

## *Nani Amsifu Mungu?*

Kwenye sura hii tunajibu kwa namna rahisi kwa kuongozwa na maandiko ya kwamba ni nani haswa anapaswa kumsifu Mungu.

Kwa mujibu wa Zaburi 148:1-12 mzaburi anaainisha wahusika waliopewa mwaliko kumsifu Mungu. Ni makundi 29 yameorodheshwa hapo:

1. Malaika wake wote
2. Majeshi yake yote
3. Jua
4. Mwezi
5. Nyota zote zenye mwanga
6. Mbingu za mbingu
7. Maji ya juu
8. Nyangumi
9. Vilindi vyote
10. Moto

11. Mvua ya mawe
12. Theluji
13. Mvuke
14. Upepo wa dhoruba
15. Milima
16. Vilima vyote
17. Miti yenye matunda
18. Mierezi yote
19. Hayawani
20. Wanyama wafugwao
21. Ndege wenye mbawa
22. Wafalme wa dunia
23. Watu wote
24. Wakuu
25. Makadhi wote wa dunia
26. Vijana waume
27. Wanawali
28. Wazee
29. Watoto

Je, wewe umo?

Umejiona kwenye orodha?

Je, unajua sasa kwa hakika umealikwa kumsifu Mungu?

Ikitokea una mashaka au bado hujawa na uhakika kwamba umo au haumo; umealikwa au la...

Zaburi 150:6

“Na KILA MWENYE PUMZI NA AMSIFU BWANA.”

Hapo umo?

Kila mwenye pumzi...; hii inatupelekea kwenye uelewa ya kwamba yake WAFU hawawezi tena kumsifu BWANA. Inachukua uwezesho wa pumzi ya Mungu ili mtu aweze kusifu.

MUNGU hatarajii kupokea sifa kutokea makaburini... ni sawa!? Hakuna mwenye pumzi huko! Hakuna uhai kutokea makaburini.

Wafu hawawezi... hawana nguvu... hawana tena hiyo shauku ya kumsifu BWANA!

MOJA YA KIASHIRIA YA KWAMBA UKO HAI NI SHAUKU, KIU, HAMU, USONGO, UWEZO WA KUMSIFU MUNGU...

Ukijiona unapoteza shauku ya kumsifu Mungu, angalia uhai wako. Angalia pumzi yako ya rohoni. Inawezekana kuna umauti umeanza kubisha hodi maishani mwako.

Si unajua hata kwa jinsi ya mwilini huwa kuna kiwango cha hewa ya oksijeni mwanadamu wa wastani anapaswa kuwa nacho kwenye mzunguko wa damu au maisha yake. Kikipungua, hiyo ni kuashiria umauti unabisha hodi. Nini mtu anafanya? Huwa anawekwa kwenye mashine ya oksijeni ili asaidike… hili ni jambo la dharula!

Kama haumsifu Mungu kibinafsi; na kama haumsifu Mungu kwenye kusanyiko la watakatifu… unahitaji kuingia chumba cha dharula usaidike.

Kwa hekima ya neno na Roho Mtakatifu pokea uhuisho wa kumsifu Mungu!

NEW VINE CHURCH | Dodoma



## Kuhusu New Vine Church

New Vine Church limebeba utume wa kuinua kizazi cha kiungu kitakacholeta mguso chanya kwenye kila nyanja ya maisha kwenye jamii, taifa na mataifa *(Mathayo 5:13-14/Yoeli 2:2-11).*

Makao makuu ya kanisa (Gloryland) yako Mwanza chini ya mwangalizi ambaye pia ni muasisi, Mchungaji Goodluck & Mama Ziada Kyara.

Kufahamu zaidi kuhusu kanisa hili kwa ujumla tembelea: https://www.newvinechurch.or.tz



---

## Mahali tulipo

Swaswa, mkabala na geti la Waziri Mkuu,
Dodoma mjini

---

## Ratiba za Ibada

| | |
|---|---|
| **Alhamis** | Saa 11.15 jioni - saa 12.15 jioni |
| **Jumapili** | Saa 3.00 asubuhi - saa 6.30 mchana |

nvc_dodoma    +255 769 240 777

## Kuhusu Mwandishi



Mwandishi wa kitabu hiki, James Kalekwa, ni mfuasi wa Yesu Kristo; mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; Mume mpenzi wa Frida, baba anayewajibika wa Joshua-Vision, Charis “Tai”, Victor na Priscilla; na anafurahia kuwa mchungaji mkazi wa kanisa la New Vine jijini Dodoma.

Mchungaji James ameitwa “Kuujaza ulimwengu kwa maarifa ya utukufu wa Mungu kama maji yaifunikavyo bahari.” [Habakuki 2:14]

## Mawasiliano na Mwandishi

wapo unahitaji kupata mafundisho zaidi ya maandishi na audios kutoka kwa mwandishi wa Kitabu hiki, Mchungaji James Kalekwa. Unaweza kufanya hivyo kupitia channel ya telegram: https://t.me/nvcdodoma AU fungua app ya telegram kisha tafuta @nvcdodoma

Unaweza pia kumfuatilia mwandishi kupitia mitandao ya kijamii:

James Kalekwa
james_kalekwa
@MchungajiJK
James Kalekwa

---

Iwapo una ushuhuda, unahitaji ushauri na msaada wa kichungaji unaweza kuwasiliana naye moja kwa moja kupitia **+255-754-917-7764** (Kupiga simu, SMS na WhatsApp).